
# Shule ya Makumu



Tusome Early Literacy Programme

# Shule ya Makumu





Shule yetu ya msingi ya Makumu ina wafanyakazi mbalimbali.

Wafanyakazi hawa hutumia vyombo vya maumbo tofauti.

Kila darasa lina ubao wenye umbo la mstatili.

Pia kuna meza, viti, kabati, milango, madirisha na makabati. Vitu hivi vilitengenezwa na fundi.





Ofisini mwa Mwalimu mkuu, mna meza ya umbo la duara.

Meza hii hutumiwa kuwekea chakula cha wageni.

Mwalimu wetu Bi. Emma hutumia tarakilishi yenye umbo la mstatili.

Kila siku, mwanafunzi bora hupewa nyota aweke kwenye tarakilishi ya Mwalimu wetu.





Shule yetu imewaajiri wapishi wawili.


Wao hutupatia chakula kwenye sahani za mviringo zenye maua ya nyota.

Shuleni, sisi hula mara tatu kwa siku.

Kila siku ya Jumanne, saa nne unusu, kila mwanafunzi hupewa sambusa yenye umbo la pembe tatu.



Baada ya chakula cha mchana, kila mwanafunzi hupewa tunda. Tunda hilo linaweza kuwa chungwa au tikiti.





Wakati wa michezo, wanafunzi hushiriki kwenye michezo mbalimbali.

Wanafunzi wengi hupenda kucheza mchezo wa mpira wa vikapu.

## Maswali

1. Ubao wa darasa una umbo gani?
2. Dirisha na kabati vimetengenezwa na nani?
3. Ofisini mwa mwalimu mkuu mna meza ya umbo gani?
4. Bi Emma hutumia tarakilishi ya umbo gani?
5. Wanafunzi hupatiwa chakula na nani shuleni?

# Shule ya Makumu

Shule ya Makumu ina wafanyakazi mbalimbali. Wao hutengeneza vitu vyenye maumbo tofauti. Pia, mna vyombo vya maumbo tofauti shuleni.

USAID
FROM THE AMERICAN PEOPLE
UKaid
from the British people

Kitabu hiki kimechapishwa kwa ufadhili kutoka kwa Shirika la maendeleo ya kimataifa la Marekani (USAID/Kenya) na Idara ya maendeleo ya kimataifa ya Uingereza (DFID/Kenya) kupitia mradi wa Tusome Early Grade Reading Activity.